# MTINDO WA JAZANDA KATIKA TAMTHILIA YA *KIJIBA CHA MOYO*

***Sophie Okwena***

IKISIRI

Makala haya yanashughulikia jazanda zilizomo katika tamthilia ya kifalsafa ya *Kijiba cha Moyo* (2009) iliyotungwa na Timothy Arege. Msuko wake unashabihiana na ule wa *Mashetani* (1971), tamthilia ya kifalsafa ya Ebrahim Hussein. Tathmini hii inaongozwa na nadharia ya kimtindo. Tumeteua kuhakiki tamthilia hii kwa msingi kwamba ni tamthilia ambayo imeandikwa kwa falsafa ya kiwango cha juu na inasheheni lugha fiche ya jazanda. Jazanda ni miongoni mwa vipengele muhimu vya lugha hivyo, matumizi mwafaka yanadhihirisha umahiri wa mtunzi. Kwa upande mwingine, matumizi chapwa ya jazanda yanaweza kuleta utata na kupotosha ujumbe wa mtunzi. Jazanda zinatumika kuleta uangavu, mvuto, ubora na utofauti wa kipekee katika kazi ya mtunzi. Aidha, jazanda ni mbinu kwasi ya usanii na mtunzi anayeitumia hufanikisha uandishi wake kwa kuendeleza maudhui na kukuza wahusika wake. Watunzi wengi hutumia jazanda kuwasilisha tajriba zao, mawazo yao na hisia zao katika vipindi na wakati wao. Kwa hiyo, sharti kuwe na uwiano kati ya ujumbe wa mtunzi na jazanda ambazo ametumia kwa sababu jazanda inapotumika katika njia mwafaka huchangia katika ufanisi wa kazi ya kisanaa kwani hutumiwa katika uzuaji na ubunifu wa kifasihi.

## 1.0 UTANGULIZI

Jazanda ni kipengele muhimu katika kazi ya fasihi. Fasihi ni sanaa bunifu ambayo hutumia lugha katika kuyasimulia maisha ya wanajamii kwa ujumla. Baadhi ya matumizi ya lugha ni ya moja kwa moja na mengine huwa fiche. Jazanda hutumia lugha fiche ambayo wakati mwingine huweza kuleta utata katika maana. Jazanda kimsingi inahusiana na taswira. Hata hivyo hutumiwa kuelezea hasa sifa za matumizi ya picha au taswira kwa ujumla wake. Tunaposema kwamba kazi fulani ina jazanda, tunalenga kwenye ujumla wa matumizi ya taswira ambazo zinaweza kuwa za aina mbalimbali (Syambo na Mazrui 1992: xvi). Jazanda inaleta picha ambayo inatufanya kuona jambo zaidi ya maana yake halisi. Upekee kuhusu lugha ya jazanda ndiyo haswa sababu inayotufanya kuipatia msisitizo au uangalifu maalumu.

Mwanafasihi hutumia ubunifu katika kuteua, kupanga na kunadi tajriba za kila aina ya maisha. Kwa hali hii, fasihi huangaliwa kama sanaa inayotumia lugha katika kueleza tajriba za wanajamii. Hivyo, kazi ya fasihi haiwezi kueleweka bila lugha kwa sababu lugha ndicho kigezo muhimu cha kupima ufanisi wa kazi ya fasihi. Kazi ya sanaa huwa na vipengele kama ploti, dhamira na wahusika, lakini bila lugha haviwezi kuwasilishwa vilivyo kwa sababu vipengele hivi hupewa umbo kupitia lugha.

Mtunzi anapotumia jazanda hulenga kupata usanii au urembo fulani kwa kuwasilisha mawazo yake kwa njia fiche na ya kuvutia kwa maneno yenye ujumi na yanayodhihirisha hisia kubwa. Aidha, matumizi ya jazanda hulenga kufikia maana mpya, pana na ya kipekee.Neno linatumika kijazanda ili kupata usanii au urembo fulani. Ikiwa tunazungumza na kuandika kijazanda, tunafanya hivyo ili kuvutia kwa

maneno yenye ujumi yanayopendeza au kudhihirisha hisia kubwa (Kovecses 2002). Waandishi wa kisanaa wanapotumia jazanda huwa na lengo la kuficha ujumbe.

Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* imeandikwa kijazanda ili kuangazia matatizo katika bara la Afrika na namna ambavyo yamewaathiri Waafrika wenyewe. Mataifa mengi katika bara la Afrika sawia na Sele (mhusika mkuu wa tamthilia hii), yamechanganyikiwa kiasi cha kutojithamini wala kujitambulisha na chochote kile. Nchi tajiri za Kimagharibi zinang'ang'ania Afrika kwa manufaa yao wenyewe bila kujali maslahi ya Waafrika na hii ndiyo sababu daktari mgeni anataka kumfanyia Sele operesheni plastia (yaani operesheni ya kuunda upya viungo - *plastic surgery)*bila kujali matokeo yake. Mataifa haya ya kibepari yamejaa ubinafsi wa hali ya juu kwa vile misaada na ufadhili wao umeambatana na masharti mabovu kama vile kustaafishwa kwa wafanyakazi mapema, kuendesha siasa za nchi maskini kwa manufaa yao na kadhalika.

Kwa hiyo, *Kijiba cha Moyo* ni tamthilia ambayo inajihusisha na masuala ya ukoloni na ukoloni mamboleo. Isitoshe, Arege anaonyesha namna Mwafrika anavyoshindwa kujithamini kwa kutumia fumbo la nyimbo tatu: wimbo wa taarab, wimbo wa *rap* (Kizungu) na wimbo wa Kichina. Sele anapowekewa wimbo wa taarabu (yaani utamaduni wa Mwafrika), anasema kwamba, haendi nao kwa sababu miondoko yake ni ya polepole hadi inamfanya ajikwae.

Hali kadhalika, Arege anajaribu kuonyesha namna mataifa tajiri yanavyonyanyasa nchi maskini kiasi cha kuwalazimisha kukubali masharti ambayo yanawaangamiza na kuwaathiri kisaikolojia bila wao kutambua. Fauka ya hayo, Arege anataka kuonyesha kuwa bara la Afrika limejaa viraka viraka kila upande, katika utamaduni, itikadi, mavazi, na kadhalika. Anaonesha ya kwamba Afrika ina kijiba (mwiba mdogo sana) ambacho kiko moyoni na ambacho si rahisi kukitoa. Jinsi ilivyo vigumu kukitoa kijiba ambacho ni kidogo zaidi katika moyo wa mwanadamu, vivyo hivyo, ni vigumu kwa bara la Afrika kujinasua kutokana na minyororo ya wafadhili wa Kimagharibi ambao nia yao sio kufadhili bali ni kujinufaisha wao wenyewe.

Ili kutimiza dhamira yake, mtunzi anatumia jazanda mbalimbali. Baadhi ya jazanda ambazo mtunzi ametumia katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* zimefafanuliwa zaidi katika makala haya.

## 1.1 Dhana ya Mtindo

Mtindo ni dhana ambayo hurejeleajinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi. Ni jinsi mwandishifulani anavyojieleza katika kazi yake. Mtindo ni tabia ya utungaji inayompambanua mtunzi mmoja na mwingine (Njogu na Chimerah 2011). Mtindo ni mtu mwenyewe yaani, jinsi mtu anavyotumia lugha kupitisha ujumbe wake na kazi ya fasihi hudumu kupitia mtindo wake na mtindo huo ni mtu mwenyewe Buffon (1930; Crystal na Davy 1969). Kadhalika, mtindo ni namna ya kujieleza kwa kutumia lugha yaani, ni namna mtunzi anavyowasilisha ujumbe wake(Ngara 1981). Nadharia ya kimtindo inaeleza kwamba, kazi ya fasihi haiwezi kueleweka bila lugha. Kwa hivyo, jinsi msanii atumiavyo lugha ndivyo husaidia kutoa ujumbe wake kwa wasomaji.

## 1.2 Kumhusu Timothy Arege

Timothy Arege ni mzaliwa wa Kaunti ya Kisii magharibi mwa Kenya. Alianza masomo yake mnamo mwaka wa 1974 katika Shule ya Msingi ya Kisii. Alisomea kuko huko katika masomo yake ya sekondari kabla ya kujiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi, ambapo alihitimu nashahada ya Sanaa katika Kiswahili na Sosiolojia. Mnamo mwaka wa 1998 alipata shahada ya Umahiri katika taaluma ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Mnamo 2012, alipata shahada ya Uzamivu katika chuo hicho hicho. Mwaka wa 2008/2009, Arege alituzwa kuwa msomi bora na Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki, Kenya. Vilevile mwaka wa 2011, Arege alishinda Tuzo ya Fasihi ya Jomo Kenyatta kwa kazi yake *Kijiba cha Moyo* (2009). Kwa sasa Arege ni mhadhiri wa somo la Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya. Tamthilia zake nyingine ni pamoja na *Chamchela* (2007) na *Mstahiki Meya* (2009).

## 1.3 Muhtasari wa *Kijiba cha Moyo*

*Kijiba cha Moyo* ni tamthilia kuhusu kijana mmoja, Sele, ambaye amekumbwa na ugonjwa usiojulikana wala kufahamika, ugonjwa ambao unahangaisha familia yake. Sele anaendelea kudidimia kiafya na kuchanganyikiwa zaidi lakini yeye yuadai kwamba si mgonjwa yu bukheri wa afya. Madaktari kadha wakiwamo madaktari Wazungu, wamejaribu kugundua ugonjwa wake lakini wote waelekea kutofahamu na wanakisia kuwa ni uchovu wa akili. Sele ni mhusika mwenye kujisaili yeye mwenyewe na pia anaisaili jamii yake. Anataka ajue nafasi yake katika jamii, na vilevile nafasi ya jamii yake katika ulimwengu, unaomilikiwa na nguvu za kibepari. Mambo yanayomsumbua ni ishara ya yale yanayoisumbua jamii pana ya taifa lake, na jamii ya Kiafrika kwa ujumla.

Tamthilia hii inaangazia uhusiano uliopo baina ya mataifa yanayoendelea yaani, mataifa machanga, hasa ya Kiafrika na yale yaliyoendelea. Uhusiano huu unaelezwa kuwa wa mnyonge na mwenye nguvu. Katika uhusiano huu, mnyonge hunyanyaswa na kudhulumiwa na mwenye nguvu kila wakati. Mataifa makuu duniani huendeleza utawala mpya wa kiuchumi uliozuka baada ya wakoloni kuondoka barani Afrika. Mataifa haya huendeleza mfumo wa kibepari (wa kikapitalisti) kupitia kwa utoaji wa ufadhili, ruzuku na katika utekelezaji wa miradi yao. Wakati kuna amani duniani, mataifa makuu huzua michafuko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa ili mataifa machanga yayakimbilie kwa usaidizi ambao hutolewa kupitia ufadhili, ruzuku, misaada na pia uwezekaji. Kwa njia hii mataifa makuu huyafanya mataifa machanga kuendelea kuyategemea.

*Kijiba cha Moyo* (2009) ni mojawapo ya tamthilia-tatizo zilizowahi kuandikwa katika fasihi ya Kiswahili. Tamthilia hii ina mtindo changamano. Ina sehemu sita, na kila sehemu ina maonyesho yake na wahusika ambao kila mmoja anaigiza nafasi yake. Tamthilia hii inawasilisha matukio na visa ambavyo ama vinaibuka au vinashawishi uhusiano baina ya mataifa yaliyoendelea na yale yanayoendelea.

## 2.0 JAZANDA KATIKA TAMTHILIA YA *KIJIBA CHA MOYO*

Tunaweza kuziweka jazanda zilizomo katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* katika makundi yafuatayo: jazanda za nyimbo tatu, pepo, bahari, kijiba, daktari, ugonjwa wa Sele, pua, uso na kovu, papa na vidagaa na wenye kushika dau. Aina hizo za jazanda zinajadiliwa hapa chini.

### 2.1 Jazanda ya Nyimbo Tatu

Arege ametumia nyimbo tatu katika tamthilia yake ya *Kijiba cha Moyo* kama jazanda. Maana ya tamthilia nzima imejikita kwenye dhana ya nyimbo tatu. Bila kupata ufasiri wa nyimbo hizo tatu, itakuwa vigumu kuelewa tamthilia nzima. Nyimbo ni msamiati maarufu sana katika mazingira ya mtunzi na nyimbo hizi zinapoimbwa huwa zinadhamiria kutekeleza majukumu mbalimbali yakiwamo kuburudisha, kuliwaza, kuelimisha, kuchangamsha, miongoni mwa majukumu mengine.

Mtunzi ametumia nyimbo kijazanda akiwa na lengo mahususi la kuwasilisha ujumbe mzito katika jamii. Wimbo wa kwanza ambao Aisha anamchagulia Sele, ni wimbo wa taarab. Wimbo huu unasimamia utamaduni wa Mwafrika, utamaduni ambao unatishia kupotea. Sele anapowekewa wimbo wa taarab, anaacha kuucheza kwa kudai kuwa mwili wake haupatani na mahadhi ya wimbo kwa sababu, wimbo wenyewe ni taratibu mno na kila anapoucheza anajikwaa. Hali hii inadhihirisha namna ambavyo Mwafrika anaendelea kuasi utamaduni wake kwa kuiga ule wa Kimagharibi. Haya yanadhihirika katika tamthilia kama ifuatavyo:

Aisha: …Tuanze na ngoma gani?
Sele: Upendayo wewe.
Aisha: (Anawaza. Anapekuapekua kaseti.Anachagua moja. Anamwonyesha Sele.) Labda hii.
Sele: Hiyo ndo gani?
Aisha: Kaseti moja ya taarab.
Sele: Taarab?
Aisha: Naam…
Sele: Haya basi… wanaanza kucheza… Sele anasimama.
Aisha: Mbona hivyo tena? Au hukuupenda wimbo.
Sele: Hata! Wimbo mzuri
Aisha: Cha mno ni nini basi? …
Sele: …Mwili wangu haupatani na mahadhi ya wimbo. Taratibu mno! Kila nikicheza muziki wa taarab, ninajikwaa. Nimeshazoea hii miziki yenye kasi. Naipenda taarab ila sipatani nayo ukumbini. Imeniasi. Au niseme mimi… mimi nimeiasi. (Uk 7-8).

Sele anawekewa wimbo wa pili wa *rap*. Wimbo huu unawakilisha utamaduni wa Kimagharibi. Anaufurahia na kuucheza kwa muda na ghafula anaacha kuucheza wimbo wenyewe. Sele anadai kwamba anakokotwa na wimbo na kwamba mwimbaji

anafokafoka anapoimba na ni kama mwenye kutoa amri kwa kiburi. Sele anaona kwamba amri yenyewe ni utumwa na anadai kuwa hataki kuwa mtumwa hata katika wimbo. Wimbo huu wa pili unasimamia utamaduni wa Kimagharibi ambao umejaa amri na masharti ambayo lazima yatimizwe na nchi maskini.

Aidha, Aisha anapojaribu kumwekea wimbo unaosema *New Kid on the Block*, Sele anadai kuwa huo pia ni utumwa kwa sababu ya maneno katika wimbo huo. Maneno yenyewe ni ya kizungu ambayo yanawakilisha utamaduni wa Kimagharibi. Maneno haya ni ishara ya vile ambavyo Mwafrika amegeuzwa kuwa mtumwa na mkoloni ingawa yuko kwao Afrika, jambo ambalo linamfanya Sele kukataa kuucheza wimbo wenyewe.

Wimbo wa tatu ni wa 'Yini Yueni' ambao Sele anaufurahia kwa kudai kwamba hauna makeke na ni wenye kuridhisha nafsi. Wimbo huu unawakilisha nchi ya Uchina. Wimbo huu unaonyesha namna nchi ya Uchina na nchi za Kimagharibi zinavyong'ang'ania nchi za Afrika kwa kisingizio cha kuleta suluhisho kwa shida zao kumbe ndizo zinanufaika zaidi.

Nyimbo hizi tatu zimetumika kijazanda kuonyesha namna Mwafrika asivyojithamini hata kidogo na hii ndiyo sababu inayomfanya Sele kudai kwamba, wimbo wa taarab unamfanya ajikwae kwa sababu ni taratibu mno. Sele anapowekewa wimbo wa pili wa Kimagharibi, anaanza kucheza japo hapatani nao vizuri. Sele anaucheza wimbo huo mpaka anajisahau. Ghafla anaacha kucheza akidai kwamba, ngoma ni nzuri yatesa mwili lakini bado moyo haulainiki. Unakuwa mgumu. Hali hii kijazanda inaonyesha namna nchi za Kiafrika zinavyofurahia misaada ya Kimagharibi bila kujua masharti ambayo yameandamana nayo. Nchi hizi za Kiafrika zinapogundua masharti haya, ambayo ni pamoja na kustaafishwa mapema, zinaanza kujinasua polepole.

Wimbo wa tatu ambao ni wa Kichina unamfanya Sele kuridhika kwa sababu hauna makeke mengi jinsi anavyodai. Hali hii kijazanda inadhihirisha ule mkondo ambao nchi za Afrika zimechukua. Mkondo wa kuruhusu Uchina kuendesha shughuli za kiuchumi katika nchi zao, jambo ambalo nchi za Kimagharibi hazijafurahishwa nalo. Hii ina maana kwamba, Uchina na nchi za Kimagharibi zinang'ang'ania Afrika, ikiwamo Kenya.

## 2.2 Jazanda ya Pepo

Dhana ya pepo imetumika kijazanda vile vile. Pepo inamaanisha nguvu zisizo za kawaida. Nguvu hizi zinaweza kuwa mbaya na hata kusababisha maafa katika jamii. Pepo hawa huogofya sana, na wanapoingia katika jamii sharti watulizwe au wafanyiwe kafara ili kuzuia maafa katika jamii.

Arege ametumia pepo kurejelea sera na nguvu zinazosimamia nchi za Afrika kutoka mbali. Nguvu hizi ni pamoja na masharti ambayo nchi maskini huwekewa na nchi tajiri za Kimagharibi. Mataifa yenye uwezo hutoa misaada kwa mataifa maskini kwa masharti fulani. Baadhi ya masharti ni kama vile kustaafishwa mapema kwa wafanyakazi, kutumia sera zao kuongoza mataifa maskini na kadhalika. Haya yanadhihirika hapa chini:

Sele: … Pepo hutoka baharini na hawatulii. Pepo… pepo hutua mahali taratibu na kuondoka vivyo hivyo tena.

Aisha: Haya yote umeyatoa wapi? Umekuwa kuhani? …

Sele: Sikuyapata haya popote. Nimeyaona, na yangu mawili. (Uk 5)

Kutokana na mazungumzo haya inabainika wazi kwamba, pepo hutua mahali taratibu na kuondoka vivyo hivyo. Hii ina maan kwamba, masharti haya huja kwa njia ambayo haieleweki moja kwa moja. Hali hii hutokea wakati mataifa maskini yanapopokea misaada ambayo huwa imeambatana na masharti, bila mataifa hayo kugundua moja kwa moja kwamba yananaswa. Haya yanadhihirika katika majibizano yafuatayo baina ya Bi. Rahma na Sele:

Bi. Rahma: …hata kama azma yenu kurudi kazini ilizimwa, haifai hivi unavyofanya wewe.

Sele: Sikiliza bibi, hivi ninavyokaa hapa nyumbanisi kwamba nimekata tamaa. La hasha! Ninajaribukutafakari kwa makini uhusiano baina yao na sisi. Na vile vile kudadisi sisi ni nani katika uhusiano huo.

Bi. Rahma: Wao sio tofauti na wewe. Ndugu zenu ndio waliowaachisha kazi na walipofanya hivyo wana sababu. Sisi hatuwezi kuzifahamu.

Sele: Hata si wao waliotuachisha. Wanatuhitaji lakini wamepewa amri na ndugu zetu washirika kupitia mikopo yao.

Si habari ya sisi kuchagua.Ni sisi tutii. Tutii amrizao mpaka lini? Uk (28, 29)

Kulingana na mazungumzo kati ya Sele na Bi. Rahma, tunabaini yale masharti ya Kimagharibi jinsi yanavyofanya kazi katika nchi maskini.Mataifa ya Kimagharibi yameweka masharti yao na kutumia sera zao katika kuongoza nchi maskini za Afrika. Masharti haya na sera hizi zao ni za kikoloni. Masharti haya ndiyo yanayoendelea kuumiza nchi maskini za Afrika. Aidha, Masharti haya ndiyo yanayotumika kustaafisha wafanyakazi mapema, jambo ambalo limeangamiza na kuvunja familia nyingi Afrika.

## 2.3 Jazanda ya Bahari

Bahari huchukuliwa kuwa na kina kirefu sana na maji mengi ambamo wanyama mbalimbali huishi. Kati ya hawa wanyama kuna wale ambao ni wazuri kwa chakula kama samaki. Hali kadhalika, ndani ya hiyo bahari kuna wanyama ambao ni hatari kama kiboko.

Arege ametumia bahari kurejelea mataifa tajiri ya Kimagharibi. Jinsi bahari inavyoweza kusakama kila kitu, ndivyo mataifa haya yenye uwezo yalivyosakama nchi maskini na kuzifanya kuwa chini yao. Mataifa haya tajiri yana tamaa wala hayatosheki, kama ambavyo bahari hubeba maji mengi wala hakuna wakati bahari imekataa kupokea maji. Hii inaonyesha uwezo wa mataifa ya Kimagharibi kwa vile mataifa haya huongoza mataifa maskini kutoka kwao. Hayayanadhihirika kama ifuatavyo:

Aisha: Naona leo twende tukaogelee.
Sele: (Ananywea kidogo) Wewe nenda. Mimi siendi baharini tena.
Aisha: Mbona usiende baharini?
Sele: Bahari ina mengi. Naigopa.Naiambaa.
Aisha: (Anamtazama kwa mshangao) Unaiogopea nini? Si mahala pakujipumbaza na kujistarehesha?
Sele: Siku hizi hata watu huangamia mumo humo baharini.Wanapigwa dafrao na maji kwa namna isiyoeleweka…
(Uk 2-3)

Aidha, yaelekea kwamba, bahari ni mataifa yaliyoendelea kama Marekani ambayo yamekusanya watu kutoka nchi mbalimbali kwa lengo la kuwapa uraia na kufanya kazi pale. Kazi ambazo watu wa nchi hizi maskini hufanya ni zile za hadhi ya chini kabisa na hata muda wa kupumzika hawana. Watu hawa hufanya kazi kwa saa nyingi sana kwa sababu gharama ya maisha ni ya juu sana. Kwa hiyo, mataifa haya yenye uwezo yana lengo la kutumia mataifa maskini kwa manufaa yao. Haya yanadhihirika hapa chini:

Sele: …Na ukiangalia kwa maakini utaona kuwa bahari inakuwakama kibakuli kidogo kinachowakusanya samakiwote pamoja. Kibakuli hiki huwa ni chambo tucha kuvivuta vidagaa karibu na papa.
Aisha: Aaaah!
Sele: Kama huamini ulizia. (Uk 38-39).

Katika mazungumzo haya bahari inalinganishwa na kibakuli kidogo ambacho kinakusanya watu kutoka sehemu mbalimbali kupitia *Green Card rotary* kwa lengo la kupata watumwa wa kufanya kazi za hadhi ya chini. Arege anajaribu kutuonyesha jinsi mataifa ya Kimagharibi yalivyo na ubinafsi mwingi kupitia kwa wahusika kama Daktari na Sele. Mataifa ya Kimagharibi ndiyo yanayoendeleza ukoloni barani Afrika. Sera zao ndizo zinazoongoza nchi maskini za Afrika.

## 2.4 Jazanda ya "Kijiba cha Moyo"

Arege ametumia anwani yake 'Kijiba cha moyo' kimafumbo. Kijiba ni mwiba mdogo.Kijiba cha Moyo ina maana ya kijiba kidogo zaidi katika moyo wa binadamu. Kijiba hiki kimedunga na kusalia katika moyo wa mwanadamu na si rahisi kukitoa. Kijiba hiki kinakuwa kisumbufu kwa moyo kiasi cha kutompa mtu utulivu hata kidogo. Tujuavyo, mwiba unapomdunga mtu mguuni, husababisha usumbufu sana kiasi hata cha kuweka usaha, na usipotolewa, huweza kusababisha madhara zaidi. Sembuse kijiba katika moyo wa binadamu, moyo ambao ndio injini na uhai wa mtu?

**Comment [PM1]:** Hakikisha usahihi wa maele – kijiba ni mwiba mdogo???

'Kijiba' kinarejelea tatizo la Mwafrika. Jinsi inavyokuwa vigumukukitoa kijiba ambacho ni kidogo zaidi katika moyo wa mwanadamu, vivyo hivyo, ni vigumu kwa bara la Afrika kujinasua kutoka katika minyororo ya wafadhili wa Kimagharibi

ambao nia yao sio kufadhili, bali ni kujinufaisha wao wenyewe. Kijiba ni tatizo la Mwafrika ambapo Mwafrika amezugwa na kuathiriwa na utamaduni wa Kimagharibi. Tatizo la Mwafrika ni kwamba, hana kitu cha kumtambulisha, ametiwa viraka viraka tu, sio kwa utamaduni wake tu bali hata itikadi yake, mila, mavazi, na kadhalika.

**2.5 Daktari kama Jazanda**

Daktari anachukuliwa kama mtu ambaye anatoa tiba na tumaini kwa mgonjwa. Mgonjwa anapomwendea daktari huwa na matumaini ya kushughulikiwa na kupona. Hata hivyo, daktari ametumika hapa kitashtiti.

Mtunzi ametumia dhana ya daktari kwa lengo tofauti na lile linalofahamika na watu. Daktari ametumika kurejelea ubinafsi wa Mzungu katika kuendesha biashara zake za kibinafsi barani Afrika ili kujitajirisha. Daktari anayetaka kumtibu Sele ni daktari wa kigeni ambaye haja yake ni pesa wala sio maslahi ya mgonjwa. Hii ndiyo sababu hataki kumweleza Sele ukweli wa kile anachotaka kufanyiwa. Sele alikuwa anataka kufanyiwa utengenezaji upya wa viungo yaani, *plastic surgery* operesheni ambayo ingeleta madhara katika mwili. Haja ya daktari huyu ni pesa; sababu hii ndiyo inayomfanya akereke na maswali ya Sele wakati Sele anamdadisi ili kujua ukweli.

Waaidha, Daktari mgeni anayeletwa kumtibu Sele haonyeshi kuelewa wala kujishughulisha kwa kina kulitatua tatizo la Sele. Utaaluma wake unatiliwa shaka na mtunzi wa tamthilia hii. Mtunzi anamfanya daktari wa kigeni ashindwe kuitambua shida ya Sele ili aweze kuonyesha kuwa suluhu ya matatizo ya wenyeji haiko kwa wageni bali kwa wenyeji.

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* daktari amesawiriwa kama mtu ambaye ana ubinafsi mwingi na ambaye hajali wagonjwa wala hawapi matumaini. Badala yake yeye anawakemea, jambo ambalo ni kinyume na taaluma aliyosomea. Haya yanadhihirika daktari anapomwambia Sele kwamba, aliende yeye mwenyewe kumtafuta akitaka huduma zake kwa hiyo Sele aamue mwenyewe. Hii ndiyo sababu anamwambia kwamba, gharama itaongezeka kwa kila huduma atakayohitaji kufanyiwa. Aidha, ubinafsi na tamaa ya daktari inadhihirika wazi wakati Sele, baada ya kutoridhirika na huduma na kutaka kurudishiwa pesa zake, daktari anamwambia kwamba atampatia tu asilimia tano. Mazungumzo yafuatayo yanadhihirisha zaidi jinsi daktari alivyojaa ubinafsi na tamaa:

| | |
|---|---|
| Sele: | …hata sasa sina ugonjwa. Siumwi popote. |
| Daktari: | Unaumwa! |
| Sele: | Siumwi. |
| Daktari: | Najua unaumwa. |
| Sele: | Ikiwa ni hivyo sitaki mambo haya tena. Nirudishie *deposit*yangu niende. |
| Dakrari: | Uliyasoma maagano? |
| Sele: | Kiasi. Sio yote. |
| Daktari: | Tutakurudishia asilimia tano kwa kukiuka maagano. |
| Sele: | Nilijua tangu hapo kwamba kipo kitu. NilihisiKwamba utanichezea ila sikutaka kukushuku kabla ya kushuhudia. Sasa |

> nimeshuhudia…sasa najua hukuja kunijali. Umekuja kwa manufaa yako uliyoyaficha… (uk55-56).

Daktari wa Kizungu anaharakisha kutaka kumfanyia Sele upasuaji plastia bila kwanza kubaini chanzo cha Sele kuchukia ngozi au hali yake ya kimaumbile. Daktari huyu ambaye amehitimu katika taaluma yake ya udaktari anataka kutibu dalili ya ugonjwa badala ya kutibu chanzo cha ugonjwa huo. Hili ni dhihirisho la jinsi Wazungu wasivyowathamini Waafrika. Tunapomlinganisha daktari huyu wa Kimagharibi na daktari Jamila ambaye ni Mwafrika, tunaona tofauti kubwa sana. Jamila ambaye amehitimu na stashahada tu, anagundua chanzo cha ugonjwa wa Sele na kuelezea familia yake kwamba, kuna dawa ya kutibu hali kama hiyo isipokuwa inachukua muda na inahitaji uvumilivu. Maelezo ya Jamila yanadhihirika hapa chini:

> Bi. Rahma: (Kwa mshangao.) Ushetani?
> Jamila: Hata!
> Bi. Rahma: Ushirikina?
> Jamila: Hapana. Ni kutoridhika na kutoikubali nafsi yako mwenyewe. Unajiona dhaifu.Unahisi unahitaji badiliko fulani. Lakini badiliko linalofanywa huwa si la nje. Wengi hawatambui kuwa tatizo limo ndani…
> Zainabu: Katika fikira.
> Jamila: ...hasa ni katika moyo. Moyo hauridhiki na siku zote kwa Kuwa Moyo ni mfalme, huamrisha fikira kutafuta suluhisho…
> Bi. Rahma: Huo ni ugonjwa gani?
> Jamila: … unajulikana katika lugha ya utabibu kama Body Dysmorphic Disorder yaani B.D.D. Ni hali ya mtu kujikuta kutopenda sehemu fulani ya mwili wake na kuichukia…
> Zainabu: Ipo dawa ya kuurai moyo kujikubali? (uk 90, 91)

Sele anasumbuliwa na fikra alizonazo kuhusu ubepari wa madola makuu duniani, hali ambayo inapingana na maisha ya kiutu. Kwa hivyo kuumwa kwake si maradhi bali kuko akilini mwake. Hii ndio sababu daktari hawezi kutambua wala kutibu ugonjwa wake kwa kuwa unatokana na mifumo ya kibepari inayoendelezwa na daktari mwenyewe. Hii ndiyo sababu katika ndoto Sele anawaona madaktari wa kigeni wakiwa wanaukimbilia na kuung’ang’ania moyo wake.

### 2.6 Jazanda ya Kovu, Uso na Pua

Sele anadai kwamba hapendipua, uso wala kovu liliopo usoni pake. Hali hii kijazanda ni kasumba na athari ya Kimagharibi. Athari ambayo imemfanya mtu mweusi kutojithamini na kujiona duni. Kasumba ya kikoloni ndiyo inayomfanya Sele kutaka kufanyiwa ugeuzaji upya wa viungo yaani *plastic surgery*. Tamthilia hii inadhihirisha athari ya elimu ya Kimagharibi miongoni mwa Waafrika na kuonyesha jinsi elimu hii ilivyoumbua utu wa Mwafrika na badala yake ikaumba kasumba ya kikoloni akilini mwake.Maelezo haya yanathibitishwa na dondoo lifuatalo:

SELE: Ni kama nilivyokuambia. Sipendi hilikovu. Uso kwa jumla. Vyote hivi vinausumbua moyo wangu. Lakini watu wanafikiri kuwa ni kuachishwa kwangu kazi kunakonisumbua… Mimi ninajielewa tofauti na wanavyonielewa. Lakini langu ni hili moja! Sipendi mkao wa uso wangu. Ninauchukia. Unanikera. Sipendi pua hii…Pua mbaya hii… (*uk*: 33-34)

Kulingana na King'ei (1987), wakoloni walijitayarishia tabaka la wenyeji lililokuwa na mwelekeo sawa na wao kupitia elimu na dini kabla ya kutoa uhuru. Maoni ya King'ei yanashadidimazungumzo yahapo juu kwakuoonyesha jinsi Mwafrika alivyoathiriwa na ugeni akawa hawezi kujithamini binafsi na hali yake kwa ujumla. Mwafrika akawa ametiwa viraka kila upande. Si itikadi, si mavazi na kugeuzwa kikaragosi cha mkoloni.

**2.7 Jazanda ya Ugonjwa**

Ugonjwa kijazanda unarejelea shida au matatizo. Ugonjwa unaomkumba Sele ni matatizo ambayo yamesababishwa na mgongano wa nafsi zake mbili zinazokinzana. Yeye anajua kwamba kuna kasoro fulani katika jamii anamoishi iliyosababishwa na kuwako kwa nguvu za kikoloni. Nguvu hizo huamua mkondo wa kisiasa na kiuchumi katika taifa lao lililo 'huru'. Isitoshe, anaelewa kuwa mataifa ya kibepari huonea na kunyanyasa mataifa machanga kwa kuingilia njia za uzalishaji na ugavi wa mali ya mataifa yao.

Ugonjwa wa Sele unaashiria matatizo yanayokumba mataifa machanga ya Kiafrika yanayosababishwa na kuwako kwa ukoloni mamboleo. Matatizo haya ni ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kadhalika. Ugonjwa wa Sele kutogunduliwa na kutibiwa kijazanda ina maana kwamba, matatizo ya Afrika bado hayajapata suluhu au hayajatatuliwa bado. Kule kukataa kwa Sele kwamba yeye si mgonjwa na wala haumwi, ina maana kwamba nchi za Afrika zimekataa kukubali kwamba zina matatizo ya kiuchumi na ya kisiasa. Haya yanathibitishwa na mazungumzo yafuatayo kati ya Sele na Bi Rahma ambaye ni bibiye Sele.

Bi. Rahma: Mimi nimepata salamu kwamba Sele mgonjwa. Nikasema, "Mume wangu mgonjwa na mimi sina habari." Basi Nikaona nije nikuone.
Sele: Vizuri umefika. Lakini hata sina ugonjwa.Mimi mzima.
Bi. Rahma: Mzima?
Sele: Mzima mimi. Mzima kama kigogo. Bukheri waafya kabisa. (uk 27)

Kulingana na muktadha wa maneno haya, ina maana kwamba, nchi za Afrika zingali zinaendelea kukana kwamba zina matatizo hasa ya kisiasa. Ugonjwa wa Sele ambao unahangaisha kila mtu katika familia yake ndilo hasa tatizo linalorejelewa hapa.

Mtindo huu wa jazanda ya ugonjwa unashabihiana na ule wa mwandishi mkongwe na maarufu, Ebrahim Hussein ambaye ametumia jazanda ya ugonjwa.Ugonjwa wa Kitaru ni wa kijazanda kwani yuko mbioni kujaribu kuelewa ubepari uliopo katika jamii yake. Aidha, anataka kujua ukweli uliosababisha tofauti

za kiuchumi, kijamii na kisiasa baina ya tabaka la kinaizi na lile la kibwanyenye. Kwa hivyo ugonjwa wa Kitaru ni fikira alizonazo kuhusu vile anavyoweza kutoka katika hali hii ya ukabaila na kisha aweze kujenga uhusiano ulio na maana.

## 2.8 Jazanda ya Papa na Vidagaa

Papa na vidagaa ni aina ya samaki ambao hupatikana katika mito, maziwa, bahari n.k. Mara nyingi viumbe hawa hutumika kama chakula. Papa ni samaki mkubwa ilhali kidagaa ni samaki mdogo sana. Mtunzi ameteua samaki hawa ambao wanafahamika sana ili kuwasilisha ujumbe mzito katika jamii. Papa anawakilisha nchi tajiri za Kimagharibi na vidagaa wanawakilisha nchi maskini za Afrika. Sele anadai kwamba michafuko mikubwa inayoifanya bahari kunguruma huvitia kiwewe vidagaa ambavyo hutafuta usaidizi wa papa lakini baadaye huliwa na papa. Hii ina maana kwamba, nchi maskini zinapokumbwa na matatizo ya majanga na ya kiuchumi, hukimbilia nchi zenye uwezo ambazo ni papa. Nchi hizi hutumia fursa hiyo kunyanyasa nchi hizi maskini. Mazungumzo yafuatayo yanathibitisha haya:

Sele: …Ni kweli papa ana kiburi kikubwa maana mfalmewa bahari.Mwili wake una uwezo wa kuzuia mawimbiya bahari navyo vidagaa hujificha nyuma yake kujisetiri. Vidagaa vinajua ni hatari lakini afadhali hatariya papa kuvila badala ya kuangamizwa na mawimbi makali. Wajua ni kama kuku ambaye anakiona kisu cha mchinjaji afadhali kuliko maisha vichakani. Na wala usisahau kuwa pumzi za papa katika vile vina virefu ni pumzi za uhai kwa vidagaa. Vidagaa hupata hewa ya kuvuta kutokanana mipumuo ya papa katika bahari kuu.

Aisha: Si kweli. Sayansi inaonyesha kuwa hayo unayosema si kweli.

Sele: Sayansi ni sayansi. Na haya ya vidagaa na papa ni ya vidagaana papa. (uk 37)

Kutokana na mazungumzo haya, nchi zenye uwezo na utajiri kama vile Marekani, zina kiburi kwa sababu zinajua kwamba ndizo tegemeo la nchi maskini. Nchi maskini hutegemea nchi hizi zenye uwezo kwa misaada ya kifedha, chakula na mikopo ambayo huandamana na masharti. Pumzi ambayo kijazanda ni misaada, ni uhai wa nchi maskini. Bila misaada huenda nchi maskini zikaangamia kiuchumi na kukumbwa na njaa.

## 2.9 Jazanda ya Wenye Kushika Dau

Arege ametumia jazanda ya wenye kushikwa na dau akiashiria raia wa taifa fulani lililohuru. Kadhalika anatumia jazanda ya wenye kulishika dau kumaanisha viongozi wa taifa hilo. Mtunzi huyu anaonyesha kuwa kila mara raia na viongozi wake huchukuliwa kama washika dau hadi pale wanapoelezwa na mtu mwingine (mkoloni mamboleo) kuwa kuna wenye kulimiliki lile dau na wanadhibiti maongozi ya dau lile. Vifungu vifuatavyo vinashadidia maelezo haya.

ZAINABU: Pamoja na hayo, sisi vilevile ni washika dau. Ingefaa kutushirikisha mapema.

MUSA: Wajua katika dau, kuna wenye kulishika na wenye kushikwa na dau. Na wakati mwingine dau tofauti si dhahiri. Kwa ujumla huchukuliwa kuwa wote wanaoliabiriani washika dau mpaka pale anapotokea mtu nakueleza kuwa wenye dau wapo na wamelitia mkononi. (*uk* 24-25)

Katika bahari kuu, mataifa haya hutatizwa na nguvu za kibepari ambazo hutishia kuyaangamiza. Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* dau na vilivyomo hudhibitiwa na nguvu za wenye dau na ambao ndio huamua ni upande upi dau lile lielekezwe.

Kutokana na jazanda hizi, inabainika kuwa kuna mtagusano kati ya raia na viongozi wa mataifa ya Kiafrika kwa upande mmoja na mataifa ya kibepari kwa upande mwingine. Katika mahusiano ya namna hii, mataifa ya kibepari hudhibiti sera za kiuchumi na siasa za mataifa machanga. Uhusiano huu umefafanuliwa na mtunzi wa tamthilia hii kuwa ni wa mwenye nguvu mpishe. Jazanda za dau, wenye dau, walioshika dau, na walioshikwa na dau zimetumiwa na Arege katika *Kijiba cha Moyo* ili kukuza na kufafanua maudhui ya ukoloni mamboleo.

## 3.0 HITIMISHO

Makala haya yametathmini matumizi ya jazanda katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*. Timothy Arege ameandika tamthilia hii ili kuangazia matatizo ya bara la Afrika na namna ambavyo matatizo haya yamewaathiri Waafrika wenyewe. Afrika sawia na Sele, ni bara ambalo limechanganyikiwa kwa sababu halijithamini wala halijitambulishi na chochote kile. Aidha,tamthilia hii ni taswira ya mataifa mengi barani Afrika ambayo yamechanganyikiwa sawa kama Sele. Waaidha, tumehakiki jazanda alizotumia mtunzi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*. Uchanganuzi umeonyesha kwamba, Arege ametumia jazanda hizi kuhuisha na kuficha ujumbe wake kwa lengo la kufikia malengo mwafaka katika uandishi wake. Aidha jazanda hizi zimetumika kuwasilisha ujumbe mzito wa mtunzi kwa wasomaji wake. Hali kadhalika, makala haya yamebainisha kwambajazanda mbalimbali zinajitokeza katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* hususan, jazanda ya nyimbo tatu, jazanda ya pepo, jazanda ya bahari, jazanda ya kijiba, jazanda ya daktari, ugonjwa wa Sele, jazanda ya pua, uso na kovu, jazanda ya papa na vidagaa na jazanda ya wenye kushika dau. Katika kuzihakiki jazanda hizi, utafiti umedhihirisha jinsi Arege anavyozitumia jazanda hizi kuendeleza msuko, wahusika na maudhui ya tamthilia yake.

## MAREJELEO


Alembi, E. (1999). *Understanding Poetry*. Nairobi: Acacia Printers Ltd.

Allen, J. W. (1971). *The Customs of Swahili People*. Berkeley: University of California Press.

Antony, D. H. (1983). Culture and Society in Town Transition: A People's History of Dar es Salaam. 1865-1939. PhD dissertation, University of Wisconsin.

Arege, T. (2007).*Chamchela*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Arege, T. (2009).*Mstahiki Meya*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Limited.

Arege, T. (2009).*Kijiba cha Moyo*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Bates, E. (1976). *Language and Context*. NewYork: NewYork Academic Press.

Coombes, J. (1953). *Literary Criticism*. London: Penguin Books.

Crystal D. and Davy D. (1969). *Investigating English Style*. London: Longman Group Ltd.

Cuddon, J. A. (1997). *A Dictionary of Literary Terms and Literary Theory*. Oxford: Blackwell Publishers.

Daiches, D. (1981). *Critical Approches to Literature*. London: Longman.

Gerald, A. (1981*). Afrcan Language Literatures*. Assex: Longman.

Gleeson, P. (1968).*Language and Culture*. Ohio USA: Charles E.

Merrill Publishing Company.

Khatib, M. S. (1992). *Taarab Zanzibar*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Habwe, J. na Matei, A. (2006). *Darubini ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix.

Harries, L. (1962). *Swahili Poetry*. Oxford: Clarendon Press.

Holman, C. (1972). *A Handbook to Literature*. New York: Macmillan Publishers

Holman, C. (1994). *A Concise Glossary of Contemporary Literary Theory*. New York: Macmillan Publishers.

King'ei, K. (2005). Swahili Taarab: From Traditional Orality to a Globalized Art Form. Lwat, A Journal of Contemporary Research, Vol 2, (2005. Pp. 1-15)

Knappert, J. (1972). Swahili Songs. *Afrika Und Ubersee* 50(3): 163-172

Kramsch, C. (1993) *Context and Culture in Language Teaching*. New York: OUP

Kulenga, C. (1977) *Tamathali za Usemi*. Dar es Salaam: East Africa Literature Bureau.

Lukacs, G. (1962). *The Meaning of Contemporary Realism.* London: Merlin Press.

Lukacs, G. (1979). *Writer and Critic and other Essays*. London: Merlin Press.

Makward, E. (1972). *Contemporary African Literature*. New York: Random House.

Mbatiah, M. (2001).*Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mbatiah, M. (2002). "Hatua za Maendeleo ya Uhakiki wa Fasihi Nchini Kenya" katika Inyani Simala, (Mh). *Utafiti wa Kiswahili*, Eldoret: Moi University Press.

Mbunda, M. (1993).*Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers Ltd

Miruka, O. (1999). *Oral Literature*. Nairobi:Acacia Publishers Ltd.

Mlacha, S. na Hurskainen, A. (1985).*Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Saalam: TUKI.

Mlama, P.(1985*)*.*"*Utunzi wa Tamthilia Katika Mazingira ya Tanzania*"Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI.

Mohamed, S.A (1995).*Kunga za Nathari ya Kiswahili*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Mulokozi, M. M. (1982). Protest and Resistance in Swahili Poetry, 1600-1885. *Kiswahili* 49 (1): 25-51.

Njogu na Chimerah (1999).*Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi:JKF.

Senkoro, F.E.M. (1977).*Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: OUP.

Senkoro, F.E.M. (1982).*Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publishing Centre.

Senkoro, F.E.M. (1987).*Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: OUP.

Wafula, R.(1999).*Uhakiki wa Tamthilia. Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: JKF.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007).*Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Routledge Publishers.

Wamitila,K.W. (2002).*Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Phonex Publishers.

Wamitila,K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.